# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## OFISI YA RAIS-TAMISEMI

**HALMASHAURI YA WILAYA CHATO**

**Namba za simu**
Mkuu wa Shule ***0752252427***

Makamu Mkuu wa Shule 0742771996 /0768402177

***Email:zakiasec@gmail.com***

SHULE YA SEKONDARI ZAKIA MEGHJI,
S.L.P 210,
**CHATO – GEITA**

---

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi………………………………
S.L.P ……………
……………………

**YAH: MAELEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI ZAKIA MEGHJI ILIYOPO HALMASHAURI YA WILAYA CHATO, MKOA WA GEITA KWA MWAKA WA MASOMO ………..**

Ninayofuraha kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii mwaka **…….** tahasusi ya EGM/HGE. Tunampongeza na karibu sana Shule ya Sekondari Zakia Meghji.

**<u>MAHALI SHULE ILIPO</u>**

Shule ya sekondari Zakia Meghji ipo Mkoa wa Geita, Wilaya ya Chato umbali wa kilometa 40 kutoka mji wa Chato barabara kuu ya Mwanza – Bukoba. Shule ipo pembeni mwa mji mdogo wa Muganza, pia shule ipo umbali wa kutembea kwa mguu kwa dakika tano (5) au usafiri wa pikipiki nauli ni Tsh 1,000/= kutoka stendi ya mabasi Muganza hadi shuleni.

**<u>NAMNA YA KUSAFIRI KUFIKA SHULE YA SEKONDARI ZAKIA MEGHJI.</u>**

1. Kwa wanaopitia au kuanzia safari zao Mwanza wanapanda mabasi yaendayo Bukoba au yanayoishia Muganza na kushukia Stendi ya Mabasi Muganza.
2. Kwa wanaotoka Dar es Salaam, Morogoro, Dodoma au Singida, Arusha, Moshi,na Tanga wanaweza kupanda mabasi yaendayo Mwanza/ Katoro/ Geita kisha wapande mabasi ya Mwanza-BUKOBA na kushukia Muganza, pia kuna maelekezo Zaidi ukiuliza utawala namba zipo hapo juu.
3. Kwa wanaotoka Karagwe kupitia Bukoba, watapanda mabasi yaendayo Mwanza na watashukia Muganza.
4. Kwa wanaotoka Kigoma, watapanda mabasi yaendayo Mwanza kupitia Runzewe wakifika Bwanga watashuka na kupanda magari yaendayo Chato- Muganza
5. Kwa wanaotoka Ngara kupitia Biharamulo, wakifika Biharamulo watapanda magari madogo yaendayo Muganza.
   **NB:** Wote hawa wakifika Muganza watashukia stendi ya Mabasi Muganza.

Muhula wa masomo unaanza tarehe **…………** Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni **ndani ya siku 14 kuanzia Tarehe ……….. hadi ………….**. Ukifika shuleni utapokelewa na Makamu Mkuu wa Shule na kusajiliwa katika daftari maalumu la kusajilia wanafunzi (Student Admission Register Book)

## 2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### 2.1 Sare za Shule

a. Mashati mawili meupe yenye mikono mirefu (weka nembo ya V bega la kushoto rangi ya sketi).
b. Sketi mbili (2) zinazovuka magoti kwa inch 6, rangi ya "DAMU YA MZEE ILIYOIVA rinda box moja kubwa mbele na nyuma na madogo mawili upande wa hips (tumia kitambaa cha suruali).
c. Hijab nyeupe (juba ndefu inayoficha mikono) ifanane na sare ya shule (kwa waisilamu tu)
d. Sare za michezo
   - Uje na raba na soksi/stockings za bluu
   - Bukta na t-shirt rangi ya bluu (t-shirt ya Taifa stars).
e. Uje na viatu vya shule vyeusi vya kufunga na kamba au vyenye by- cross visivyo na visigino.
f. Soksi jozi mbili nyeupe ndefu (Stockings)
g. Sweta 1 rangi ya DAMU YA MZEE iliyoiva.
h. Nguo za kushindia (Shamba dress)
   - Gauni mbili (2) rangi ya pink kitambaa Kizito (mshono ni solo).
   - Tshirt 1 rangi ya cream yenye nembo ya shule(zinapatikana kwenye maduka yaliyopo Jirani na shule kwa Tsh 15,000/=)
i. Tai 2 rangi ya DAMU YA MZEE iliyoiva kitamba cha sketi.
j. Track-suit (suruali na jaketi lake rangi ya dark blue) Sare ya kuvaa wakati wa masomo ya usiku.

**NB. Wazazi ambao upatikanaji wa sare za shule utakuwa mgumu kupatikana wawasiliane na uongozi wa shule kwa msaada zaidi.**

### 2.2 Michango ya shule

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**Mchango Wa uendeshaji wa shule ulipwe kwenye akaunti Na. 32701200048 NMB – ZAKIA MEGHJI SEC SCHOOL RECURRENT A/C**
**Michango mingine ilipwe kwenye Akaunti Na. 31702300264 NMB - ZAKIA MEGHJI SECONDARY SCHOOL PROJECT A/C.** (Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye bank pay in slip)

a. **Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni:-**

- Kila mwanafunzi aje na **BIMA YA AFYA** hivyo mzazi hakikisha mwanao anakuja na BIMA HIYO au aje akatiwe shuleni kwa gharama ya Tsh 50,400/=.
- Fyekeo, Reki na mpini wake, Mopa, soft broom **(HGE)** na hard broom (brash) jembe na mpini wake na chelewa**.(EGM).** (Vinapatikana Duka yaliyopo Jirani na shule).
- Godoro futi 2 ½
- Chandarua pembe nne rangi nyeupe.
- Ndoo mbili, moja yenye ujazo wa lita 20 na nyingine lita 10.
- Chombo chenye ujazo wa lita 5 cha kuhifadhi maji ya kunywa.
- Bakuli, sahani, kikombe, na kijiko kwa ajili ya uji na chakula.
- Kalamu za kutosha na vifaa vya kuchorea.
- Flat file kwa ajili ya kutunza kumbukumbu zako.
- Counterbooks 11 za 4Quire au 3Quire (zinapatikana kwenye maduka yaliyopo Jirani na shule)
- Ream 1 A4 kwa kila mhula wa masomo.
- Advanced Learners Dictionary kwa matumizi yako (ni ya lazima).
- Scientific Calculator.
- Hati maalumu ya vipimo vya daktari kuthibitisha hali ya afya yako (fomu imeambatishwa).

**NB: Mahitaji mengine yanapatikana kwenye maduka yaliyopo Jirani na shule, daftari, kalamu, file, calculata na vifaa vingine kwa bei nafuu.**

### 2.3 MAVAZI NA NGUO BINAFSI

- Jozi moja ya kanga.
- Taulo.
- Kanda mbili za kuogea.
- Under-skirts mbili au zaidi na nguo za ndani zisizopungua 15 na pads bunda 5.
- Shuka mbili za Blue pamoja na blanketi moja.
- Nguo za kulalia.

**NB: Mavazi ambayo sio sare ya shule hayaruhusiwi kufika eneo la shule.**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- ✞ **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi; mwanafunzi akikutwa na simu au dalili za kuwa na simu mzazi atatozwa faini kubwa sana au kufukuzwa shule, hivyo ongea na mwanao.**

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:** i. Wizi;

ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
viii. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
ix. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
x. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xi. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xii. Kudharau Bendera ya Taifa;
xiii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na

**Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali; ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;

iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na

iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

***"KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI ZAKIA MEGHJI"***

……………………………

**MFUNDA LADISLAUS MGAJU**
**MKUU WA SHULE**
***Mawasiliano 0752252427***

THE HEADMISTRESS
ZAKIA MEGHJI SECONDARY SCHOOL
P.O.Box 210
CHATO

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule : 0752252427**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0742771996 / 0768402177**
- **Mwandamizi Taaluma 0787711889**
- **Mwalimu wa malezi 0759715490**

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## OFISI YA WAZIRI MKUU-TAMISEMI
### HALMASHAURI YA WILAYA CHATO

**Namba za simu**
Mkuu wa Shule ***0752252427***
Makamu Mkuu wa Shule 0742771996 / 0768402177
***Email:zakiasec@gmail.com***

SHULE YA SEKONDARI ZAKIA MEGHJI,
S.L.P 210,
**CHATO - GEITA**

---

**MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI**

Sehemu hii ijazwe na mwanafunzi:

1. Jina kamili la mwanafunzi:……………………………………………………………………
2. (a) Tarehe ya kuzaliwa:…………………………………………………………………………
    (b) Kijiji/Mtaa alipozaliwa………………………………………………………………………
3. (a)Dini:……………………………………………………………………………………
    (b) Dhehebu:……………………………………………………………………..
4. (a) Ni raia wa Tanzania? (Jibu NDIYO au HAPANA)……………………………………………
    (b) Kama siyo Mtanzania, taja uraia wako na ulete cheti cha uraia:………………………
5. (a) Darasa ulilomaliza:………………………………………………………………………
    (b) Shule ulikotoka:…………………………………………………………………………
6. (a) Jina kamili la Baba/Mama/Mlezi:……………………………………………………………
    (b) Anwani ya Mzazi/Mlezi:…………………………………………………………………
    (c) Namba ya simu ya Mzazi/Mlezi:…………………………………………………………
7. (a) Mahali unapoishi:……………………………………………………………………………
    (b) Ni umbali gani kutoka shuleni?.............................................................................................
8. (a) Unaishi na nani? Taja jina lake kamili:……………………………………………………
    (b) Una uhusiano gani na huyo uliyemtaja?..............................................................................
    (c) Unaishi katika nyumba ya kupanga? (Jibu NDIYO au HAPANA)……………………………
9. Mzazi/Mlezi anafanya kazi gani?.................................................................................................
10. Je una ndugu Chato/Muganza? (Jibu NDIYO au HAPANA). Kama ndiyo, anaitwa nani?..................................................uhusiano ………………………..……………
    Anaishi wapi…………………………………………………………..………….
    Namba yake ya simu…………………………………………..……………….

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## OFISI YA WAZIRI MKUU-TAMISEMI
### HALMASHAURI YA WILAYA CHATO

**Namba za simu**
Mkuu wa Shule ***0752252427***
Makamu Mkuu wa Shule 0768402177
/ 0742771996
***Email:zakiasec@gmail.com***

SHULE YA SEKONDARI ZAKIA MEGHJI,
S.L.P 210,
**CHATO - GEITA**

---

**FOMU YA KUKUBALI**

**PICHA YA MWANAFUNZI**

**A: MWANAFUNZI**

Mimi ……………………………………………….. ambaye ni mwanafunzi niliyechaguliwa kujiunga na shule ya Sekondari ZakiaMeghji, nakubali kuchukua nafasi niliyopewa ya kidato cha ……………

Katika Shule ya Sekondari ZakiaMeghji. Naahidi kuwa, nitatii na kufuata sheria, taratibu na kanuni zote za shule.

| | |
|---|---|
| …………………………… | ………………………… |
| Sahihi ya Mwanafunzi | Tarehe |

---

**PICHA YA MZAZI/MLEZI**

**B: MZAZI/MLEZI**

Mimi………………………………………………….Mzazi/Mlezi wa……………………………… Nimeyasoma masharti yote ya mwanangu kujiunga na Shule ya Sekondari ZakiaMeghji.

Ninakubali na kuahidi kuwa mwanangu atafuata na kutii masharti yote ya shule. Aidha naahidi nitawajibika kwa kumlipia ada ya shule mwanangu pamoja na michango mbalimbali ya shule na nitakuwa tayari kushirikiana na shule pindi nitakapotakiwa kufanya hivyo.

| | |
|---|---|
| **…………………………** | **…………………………** |
| Sahihi ya Mzazi/Mlezi | Tarehe |

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## OFISI YA WAZIRI MKUU-TAMISEMI
### HALMASHAURI YA WILAYA CHATO

**Namba za simu**
Mkuu wa Shule ***0752252427***
Makamu Mkuu wa Shule 0768402177 / 0742771996
***Email:zakiasec@gmail.com***

SHULE YA SEKONDARI ZAKIA MEGHJI,
S.L.P 210,
**CHATO - GEITA**

**KIAMBATANISHO B**
**MEDICAL EXAMINATION FORM**

(To be completed by a medical office)
Student name ……………………………………………………………………………………
Age ………………………………………………………………………………………………
Blood examination: Haemaglobin …………………………………………………………….
Any abnormalities Notes ………………………………………………………………………
Stool examination ……………………………………………………………………………..
Urinalysis ………………………………………………………………………………………
Pregnancy…………………………………………………………………………………....
T.B Test (If negative Immunizations given) ……………………………………………………
……………………………………………………………………………………………….
………………………………………………………………………………………………..
Eyes …………………………………………………………………………………………….
Chest ……………………………………………………………………………………………
Any chronic complaints not noted above e.g.
Asthma ………………………………………………………………………………………….
Headache ………………………………………………………………………………………..
Skin disease etc …………………………………………………………………………………….
…………………………………………………………………………………………………
Also anything else that the school staff should know
About ……………………………………………………………………………………………….
…………………………………………………………………………………………………….
Any treatment given or recommended ……………………………………………………………
In case of Bilharzias it's recommended that student should attend the Bilharzias clinic before they come to school ……………………………………………………………………………………………..
I certify that I have examined the above student and recommended that she/he fit unfit to pursue Secondary education.

Signature of examiner………………..
Designation ………………………….
Official stamp ……………………
Date ……………………………

**NAMNA YA USHONAJI WA SARE ZA SHULE NA JINSI ZINAVYOTAKIWA KUONEKANA.**

Sketi mbili (2) rangi ya "DAMU YA MZEE ILIYOIVA rinda box moja kubwa mbele na nyuma na madogo mawili up ande wa hips (tuma kitambaa cha suruali)







N:B. Mavazi ya wanafunzi yapo katika muonekeano huo hapo juu, Sare tofauti na hizo hazitakubalika. Kwa msaada piga simu **0742771996.**

**Pia kutakuwa na kundi la whatsap la wazazi na uongozi wa shule kupitia namba 0742771996 ili kukupa taarifa mbalimbali za shule na wewe kutoa maoni yako. Unaombwa ujiunge na kundi hili.**